

DEMOCRATIC
REPUBLIC OF
THE CONGO

BURUNDI

TANZANIA

ZAMBIA

KATIBA KUZITA

KLABU YA UHIFADHI WA
ZIWA TANGANYIKA

ZIWA LETU • SAMAKI WETU •
MUSTAKABALI WETU



YALIYOMO

YALIYOMO	1
SURA YA KWANZA	3
1.1. Utangulizi	3
1.2. Jina la Klabu	3
1.3. Anwani ya Klabu	3
1.4. Maana na Tafsiri	3
SURA YA PILI	4
2.1. Maono	4
2.2. Dhamira	4
2.3. Malengo Mahususi	4
2.4. Shughuli Kuu za Klabu	4
SURA YA TATU	6
3.1. Sifa za Mwanachama	6
3.2. Haki za Mwanachama	6
3.3. Wajibu wa Mwanachama	6
3.4. Kujiunga na Klabu	6
3.5. Kusitisha Uanachama	6
SURA YA NNE	8
4.1. Walezi	8
4.2. Majukumu ya walezi	8
4.3. Viongozi wa Klabu	8
4.4. Uchaguzi wa Viongozi	8
4.5. Sifa na Vigezo vya Viongozi Wanaochaguliwa	9
4.6. Majukumu ya Viongozi	9
SURA YA TANO	11
5.1. Mikutano ya Klabu	11
5.2. Mkutano wa Kamati Tendaji	11
5.3. Akidi na Ajenda	11

YALIYOMO

SURA YA SITA	12
6.1. Vyanzo vya Fedha	12
6.2. Matumizi ya Fedha	12
6.3. Usimamizi wa Fedha	12
SURA YA SABA	13
7.1. Marekebisho	13
7.2. Utatuzi wa Migogoro	13
SURA YA NANE	14
8.1. Uhalali	14

UTANGULIZI, JINA, ANWANI YA MAKAO, MAANA NA TAFSIRI

1.1. Utangulizi

Hii ni Katiba ya Klabu Ya Uhifadhi wa Ziwa Tanganyika (**KUZITA**) – klabu ya uhifadhi wa mazingira ya Ziwa Tanganyika, iliyopo katika Shule ya Sekondari Kipili, Kirando na Usesula Kata ya Kipili, Kirando na Mkinga Wilaya ya Nkasi-Mkoa wa Rukwa. Klabu hii imeanzishwa kwa ridhaa ya wanafunzi kwa kushirikiana na walimu walezi, ikiwa ni jukwaa maalum la kuwahamasisha wanafunzi kushiriki kikamilifu katika juhudi za uhifadhi wa mazingira ya Ziwa Tanganyika na rasilimali zake.

Kupitia elimu, ushiriki wa vitendo na uhamasishaji, klabu inalenga kukuza uelewa kwa wanafunzi na jamii kuhusu changamoto za kimazingira zinazolikumba Ziwa Tanganyika, kuzuia uvuvi haramu, na kuendeleza matumizi endelevu ya rasilimali kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

1.2. Jina la Klabu

Jina la klabu hii ni: “**Klabu ya Uhifadhi wa Ziwa Tanganyika**” Kwa kifupi: **KUZITA**

1.3. Anwani ya Klabu

Makao makuu ya klabu yatakuwa katika Shule husika, zilizopo katika Kata ya Kipili, Mkinga na Kirando Wilaya ya Nkasi, Mkoa wa Rukwa.

1.4. Maana na Tafsiri

- i. Klabu: Kikundi rasmi cha wanafunzi kinachojishughulisha na masuala ya uhifadhi wa mazingira ya Ziwa Tanganyika.
- ii. Uhifadhi: Shughuli zinazolenga kulinda na kutunza mazingira na rasilimali za asili za Ziwa Tanganyika.
- iii. Ziwa Tanganyika: Moja ya maziwa makuu ya Afrika, linalopatikana upande wa magharibi mwa Tanzania na kuwa na umuhimu mkubwa wa kiikolojia, kiuchumi na kijamii.

MAONO, DHAMIRA, MALENGO MAHUSUSI NA SHUGHULI KUU**2.1. Maono**

Kuwa chombo cha mabadiliko chenye lengo la kulinda Ziwa Tanganyika kwa kizazi cha sasa na kijacho, kupitia elimu, ushawishi na vitendo vya uhifadhi.

2.2. Dhamira

Kuelimisha na kuhamasisha wanafunzi na jamii kuhusiana na umuhimu wa Ziwa Tanganyika na hatua mahususi za kuhifadhi mazingira na bioanuwai.

2.3. Malengo Mahususi

- i. Kutoa elimu kwa jamii kuhusu uvuvi haramu na athari zake, na kuhamasisha umuhimu wa kulinda Ziwa Tanganyika kwa ajili ya matumizi endelevu.
- ii. Kuongeza uelewa juu ya uharibifu wa mazingira, uchafuzi wa maji na mabadiliko ya tabianchi.
- iii. Kukuza ari ya ushiriki wa wanafunzi, walimu na jamii katika shughuli za uhifadhi wa Ziwa Tanganyika kupitia semina, kampeni za uhamasishaji, na kazi za vitendo.
- iv. Kuratibu na kushiriki katika shughuli za mazingira kama upandaji miti, usafi wa fukwe, na ukusanyaji wa taka kwa lengo la kuboresha mazingira ya Ziwa Tanganyika.
- v. Kuandaa mijadala, mashindano, maonyesho na ziara za kielimu za kukuza maarifa ya wanafunzi kuhusu Uhifadhi wa Ziwa Tanganyika na bioanuwai yake.

2.4. Shughuli Kuu za Klabu

- i. Kufanya kampeni za uhamasishaji na elimu shuleni na kwenye jamii juu ya athari za uvuvi haramu.
- ii. Usafi wa mazingira ya fukwe za Ziwa Tanganyika.

- ii. Usafi wa mazingira ya fukwe za Ziwa Tanganyika.
- iii. Upandaji miti katika maeneo ya mwambao wa ziwa, na maeneo mengine ya kuhifadhi mazingira.
- iv. Kufikisha ujumbe kwa njia bunifu kama vile maonesho ya picha, michoro, maigizo, nyimbo, ngonjera na insha kuhusu Ziwa Tanganyika na Uhifadhi.
- v. Kufanya ziara za mafunzo kwenye taasisi za uhifadhi wa Ziwa Tanganyika kama Beach Management Units (BMU) ili kujifunza mikakati na namna bora za uhifadhi.
- vi. Kushiriki maadhimisho ya matukio maalumu kama maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, Siku ya Uvuvi Duniani n.k.

UANACHAMA

3.1. Sifa za Mwanachama

- i. Awe mwanafunzi aliyejiandikisha Shule husika.
- ii. Awe na maadili mema na anayejali masuala ya mazingira.
- iii. Awe tayari kushiriki shughuli za klabu bila kulazimishwa.

3.2. Haki za Mwanachama

- i. Kushiriki vikao, mafunzo na shughuli rasmi za klabu.
- ii. Kupendekeza, kuchagua au kuchaguliwa katika nafasi za uongozi.
- iii. Kupokea taarifa rasmi za maendeleo ya klabu.

3.3. Wajibu wa Mwanachama

- i. Kuhifadhi mazingira ya shule, kijiji na Ziwa Tanganyika.
- ii. Kuhudhuria vikao na kutoa maoni yenye kujenga.
- iii. Kuwajibika katika kazi za pamoja.
- iv. Kutoa taarifa ya uharibifu wa mazingira kwa uongozi.
- v. Kutunza na kulinda rasilimali za Klabu.

3.4. Kujiunga na Klabu

- i. Mwanachama atajiunga kwa kujaza fomu na kuidhinishwa na uongozi.
- ii. Atapewa taratibu za awali.

3.5. Kusitisha Uanachama

Uanachama utakoma kutokana na sababu zifuatazo:

- i. Iwapo mwanachama ataamua kujitoka kwa hiari yake mwenyewe.
- ii. Utovu wa nidhamu au kushiriki uharibifu wa mazingira.

- iii. Iwapo atashindwa kushiriki katika shughuli za klabu kwa muda mrefu bila sababu maalum.
- iv. Iwapo atashindwa kuzingatia matakwa ya katiba hii.

MUUNDO WA UONGOZI WA KLABU

4.1. Walezi

- i. Kutakuwa na Mlezi mmoja wa klabu ambaye atapendekezwa, Kukubali na kuidhinishwa na Mkuu wa shule.
- ii. Mlezi anaweza kuhudumu kwa mwaka mmoja au zaidi, kulingana na utayari wake na makubaliano ya shule.

4.2. Majukumu ya walezi

- i. Kutoa ushauri kuhusu mpangilio wa shughuli za mazingira, kampeni, miradi ya uhifadhi n.k.
- ii. Kuhakikisha kuwa wanafunzi wanatekeleza shughuli kwa nidhamu na kufuata katiba ya klabu.
- iii. Kuandaa au kusaidia maandalizi ya mafunzo na warsha kwa wanachama wa klabu kwa kushirikiana na wadau wa mazingira.

4.3. Viongozi wa Klabu**4.4. Uchaguzi wa Viongozi**

- i. Viongozi watachaguliwa kila baada ya mwaka mmoja katika Mkutano Mkuu wa Klabu.
- ii. Uchaguzi utafanyika wazi au kwa kura ya siri.
- iii. Walimu walezi watasimamia uchaguzi.

4.5. Sifa na Vigezo vya Viongozi Wanaochaguliwa

- i. Awe na nidhamu na tabia njema.
- ii. Awe mwajibikaji na mpenda mazingira.
- iii. Awe na uwezo wa kuwasiliana vizuri.
- iv. Awe tayari kushirikiana na wengine.
- v. Awe mwaminifu na anayeaminika.
- vi. Awepo shuleni mara kwa mara (asiwe mtoro).
- vii. Mwenyekiti, Katibu, Mweka Hazina, kiongozi wa Nidhamu na Mratibu wa Mipango hawatakiwi kuwa wanafunzi wa kidato cha nne.
- viii. Viongozi watachaguliwa kutoka kwa wanafunzi wa kila darasa ili kuhakikisha uwakilishi mpana wa klabu.

4.6. Majukumu ya Viongozi

4.6.1. Mwenyekiti

- Kuongoza na kusimamia mikutano.
- Kusimamia utekelezaji wa shughuli za Klabu.
- Kutoa taarifa kwa walezi na uongozi wa shule.
- Kuwakilisha klabu kwenye vikao au shughuli za shule na nje ya shule.

4.6.2. Katibu

- Kuandika na kutunza kumbukumbu za mikutano ya klabu.
- Kutunza nyaraka zote za klabu (ratiba, orodha ya wanachama, taarifa).
- Kutuma taarifa za mikutano na shughuli kwa wanachama.
- Kusaidia kuandaa ripoti za shughuli za klabu.
- Kushirikiana na Mwenyekiti kupanga ajenda za mikutano.

4.6.3. Mweka Hazina

- Kutunza fedha na rasilimali za klabu kwa uaminifu.
- Kurekodi mapato na matumizi ya klabu kwa usahihi.
- Kuandaa taarifa ya fedha kwa mikutano ya klabu.
- Kushirikiana na walimu walezi na viongozi katika matumizi ya fedha.
- Kuhakikisha matumizi yote yanafanyika kwa kufuata taratibu za klabu.

4.6.4. Msimamizi wa shughuli za club

- Kusaidia viongozi wa klabu katika kupanga na kutekeleza shughuli za klabu.
- Kuhamasisha wanachama kushiriki kikamilifu katika mikutano na shughuli za Klabu.
- Kuwakilisha maoni na mapendekezo ya wanachama kwenye vikao vya uongozi.
- Kufuatilia utekelezaji wa maamuzi yaliyofikiwa na Kamati Tendaji.
- Kushiriki kikamilifu kwenye shughuli zote za klabu kama wawakilishi wa wanachama.

4.6.5. Mwenyekiti wa michezo

- kuratibu michezo yote na burudani
- Kuandaa ratiba ya mazoezi na mashindano.
- Kuhamasisha ushiriki wa wanachama.
- Kusimamia matumizi ya vifaa vya michezo.
- Kufuatilia nidhamu na usalama wakati wa michezo.
- Kuwasilisha taarifa za shughuli za michezo kwa uongozi

4.6.6 Mwenyekiti wa nidhamu

- Kusimamia na kuhakikisha wanachama wote wanazingatia katiba, kanuni na taratibu za klabu.
- Kuhamasisha nidhamu, uwajibikaji na heshima miongoni mwa wanachama wakati wa mikutano na shughuli zote za klabu.
- Kushirikiana na viongozi wengine kudumisha utulivu na mpangilio wakati wa mikutano, mafunzo na shughuli za uhifadhi wa Ziwa Tanganyika.
- Kushauri na kuelimisha wanachama kuhusu umuhimu wa kuzingatia maadili na kanuni za klabu. Kupokea na kuripoti masuala yanayohusu ukiukwaji
- Kupokea na kuripoti masuala yanayohusu ukiukwaji wa nidhamu kwa uongozi wa klabu na Mwalimu Mlezi (Focal Teacher) kwa hatua stahiki.
- Kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ya kinidhamu yaliyofikiwa na uongozi wa klabu.
- Kushirikiana na Mwalimu Mlezi na viongozi wa klabu kutatua migogoro kwa njia ya haki, mazungumzo na kuheshimu haki za wanachama.

MIKUTANO NA SHUGHULI

5.1. Mikutano ya Klabu

5.1.1. Mkutano Mkuu

- Utafanyika mara moja kila muhula.
- Kuandaa mpango kazi wa Klabu.
- Kujadili maendeleo, mipango, na changamoto.
- Kufanya uchaguzi wa viongozi.

5.1.2. Mkutano wa Kawaida wa Wanachama Wote

- Utafanyika angalau mara moja kwa mwezi au kwa kuafuta ratiba ya shule.
- Utajadili mambo ya kawaida ya maendeleo ya klabu, changamoto, mapendekezo na ratiba ya shughuli.

5.2. Mkutano wa Kamati Tendaji

- Kikao hiki kitafanyika angalau mara moja kwa mwezi au inapohitajika kwa dharura.
- Washiriki wa kikao ni viongozi wote wa klabu pamoja na walimu walezi.

5.3. Akidi na Ajenda

- Akidi ya mkutano au kikao ni angalau theluthi mbili ($\frac{2}{3}$) ya wanachama wote hai wa klabu, viongozi wa klabu na angalau mwalimu mmoja mlezi.
- Ajenda ya mkutano zitaandaliwa na Katibu kwa kushirikiana na Mwenyekiti na kuidhinishwa na Mwalimu Mlezi.
- Ajenda zitatolewa mapema kwa wanachama au viongozi angalau siku mbili kabla ya mkutano.

FEDHA NA RASILIMALI

6.1. Vyanzo vya Fedha

- i. Msaada kutoka kwa shule, taasisi za kiserikali na mashirika yasiyo ya kiserikali.
- ii. Mauzo ya bidhaa au shughuli za klabu kama bustani n.k.

6.2. Matumizi ya Fedha

Fedha za klabu zitatumika kwa shughuli za uhifadhi, mafunzo, vifaa vya elimu, usafiri (ikihitajika), na matumizi mengine yaliyoidhinishwa na kamati Tendaji.

6.3. Usimamizi wa Fedha

- i. Fedha zote za klabu zitatunzwa na Mwalimu Mlezi wa klabu kupitia mfumo rasmi uliowekwa na uongozi wa shule.
- ii. Mweka Hazina wa klabu atahusika na kurekodi mapato na matumizi, lakini hatashika fedha mkononi.
- iii. Ripoti ya kifedha itatolewa kila muhula, Taarifa ya fedha itawasilishwa kwa wanachama kila robo mwaka au muda itakapohitajika.

MAREKEBISHO YA KATIBA

7.1. Marekebisho

- i. Marekebisho ya katiba yanaweza kupendekezwa na mwanachama yeyote wa klabu kwa maandishi.
- ii. Pendekezo litajadiliwa na Kamati Tendaji na kuwasilishwa kwenye mkutano wa wanachama.
- iii. Marekebisho yatakubaliwa ikiwa yataungwa mkono na angalau theluthi mbili ($\frac{2}{3}$) ya wanachama waliopo kwenye mkutano.

7.2. Utatuzi wa Migogoro

- i. Migogoro yote ya ndani ya klabu itashughulikiwa kwanza kwa mazungumzo ya wazi kati ya wanachama au viongozi husika.
- ii. Iwapo suluhu haitapatikana, suala litaelekezwa kwa Kamati Tendaji ya klabu kwa maamuzi chini ya usimamizi wa Walezi.
- iii. Endapo bado hakutakuwa na suluhu, mgogoro utawasilishwa kwa Mkuu wa Shule.

HITIMISHO**8.1. Uhalali**

Katiba hii itaanza kutumika rasmi baada ya kupitishwa na wanachama na kuidhinishwa na Mkuu wa Shule.

Jina la mkuu wa shule

Shule.....

Saini.....

Imeandaliwa na kupitishwa walimu (waliojengewa uwezo) pamoja na wanachama wa Klabu ya Uhifadhi wa Ziwa Tanganyika – nakupitishwa na mkuu wa shule

Tarehe: _____

Saini za Viongozi wa Klabu

Mwenyekiti: _____

Katibu: _____

Mwalimu Mlezi 1: _____



IMPLEMENTED BY:
SMART Youth Effort for
Advanced Community



PROJECT:
KUZITA School Conservation
Clubs (Pilot Phase)



VERSION:
1.0



YEAR:
2026



PILOT SCHOOLS:
Kirando, Usesula and
Kipili Secondary Schools



Smart_youth_effort | www.smartyouth.or.tz